

SHIRIKA LA RELI TANZANIA

Simu: 2133990
Telegramu: Railways
Nukushi: 2133428



Ofisi ya Mkurugenzi Mkuu
S.L.P 70364
Dar es Salaam
04 Oktoba 2019

TAARIFA KWA UMMA

KUKANUSHA TAARIFA ZINASOZAMBAA KATIKA MITANDAO YA KIJAMII KUHUSU FURSA ZA AJIRA ZAIDI YA 200 ZILIZOTANGAZWA NA SHIRIKA LA RELI TANZANIA –TRC

Shirika la Reli Tanzania limebaini taarifa za upotoshaji umma katika mitandao ya kijamii na watu ambao si waadilifu kwa watanzania na kutumia sehemu za wazi kubandika matangazo katika baadhi ya maeneo tofauti hasa yenye mikusanyiko ya watu wengi juu ya fursa za ajira zaidi ya 200 hivi karibuni oktoba 2019.

Shirika la reli Tanzania linakanusha taarifa hizo zenyenye lengo la kupotosha umma na utapeli kuwa si za kweli na Shirika halijatangaza fursa za ajira katika kada yoyote hivi karibuni, hivyo wananchi na wadau mnaombwa kupuuza taarifa hizo.

Kama ilivyo katika taasisi na mashirika ya serikali, ajira zote hutangazwa kwa kufuata sheria na taratibu za kuajiri kwa kufuata miongozo ya utumishi wa umma kwa kufuata taratibu, kanuni na sheria za kazi.

Shirika linakemea vikali vitendo vyta upotoshaji wa taarifa kwa umma, kama kuna uhitaji wa taarifa zozote kuhusu TRC, unaweza fungua tovuti ya TRC na kupata taarifa za uhakika www.trc.co.tz au fungua mitandao ya kijamii “Facebook, Twitter, Instagram kwa anuani tzrailways au kutumia simu ya huduma kwa wateja ya bure ambayo ni : 0800110042.

Imeandaliwa na Ofisi ya Uhusiano kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu
Shirika la Reli Tanzania